policy forum

# MAPENDEKEZO KWA AJILI YA KATIBA MPYA YALIYOTOLEWA NA WANACHAMA WA POLICY FORUM

## UTANGULIZI (PREAMBLE)

## MISINGI YA KATIBA

Misingi ya Katiba ya sasa[1] inaainisha kuwa katiba imetungwa na Bunge kwa niaba ya wananchi kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa Tanzania inaongozwa na serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini.

Utangulizi pia unatambua jamii yetu inazingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na Amani. Pia unatambua kuwa husimamiwa na bunge lililochaguliwa na wananchi, na pia jamii yenye mahakama huru zinazotekeleza wajibu bila woga wala upendeleo.

**Tunashauri** yafuatayo yawepo pia kwenye utangulizi ili kuweka msisitizo wa misingi muhimu ya watanzania:

- Utangulizi utambue kuwa nchini Tanzania, historia inaonesha uwepo wa dhuluma pamoja na ukosefu wa usawa kwa wanawake na watu wa makundi maalum na hivyo kuna nia ya katiba mpya kurekebisha hili. Tungependa kuona kipengele mahususi kinachotaja usawa wa kijinsia kinagaubaga katika utangulizi.
- Japo utangulizi unataja na kutambua kuwa Tanzania inazingatia misingi ya uhuru, haki, udugu, amani, ujamaa demokrasia na serikali isiyokuwa na dini, imesahaulika msingi mmoja mkubwa: umuhimu wa UMOJA WA WATANZANIA wakiishi katika nchi yenye makundi, makabila, rangi nyingi.
- Tungependa msingi wa UWAZI WA SERIKALI kwa watu wake na UWAJIBIKAJI wa serikali kwa watu wake na matakwa yao yatambulike pia katika utangulizi.
- "Supremacy of the Constitution": Tunashauri utangulizi utambue katiba ni sheria mama ya Tanzania na sheria zingine zote na maamuzi yote yatakuwa chini ya katiba.

Tunaamini haya yakiwekwa kwenye utangulizi yataonesha msisitizo juu ya misingi yanayosimamiwa na watanzania.

[1] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, 2005

# SURA YA KWANZA

## JAMHURI YA MUUNGANO, VYAMA VYA SIASA, WATU NA SIASA YA UJAMAA NA KUJITEGEMEA

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inaeleza wazi kuwa Tanzania ni nchi moja na ni ya Jamhuri ya Muungano ambao unahusisha eneo lote la Tanzania bara na Tanzania Zanzibar.

Kulingana na hili, kwa sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina pande mbili: Zanzibar na jamhuri ya Muungano. Tanganyika imetoweka. Zanzibar ni nchi kamili yenye Katiba, Rais, Makamu wawili wa Rais, Waziri Kiongozi, Baraza la Mawaziri, Bunge (Baraza la Wawakilishi), Wimbo wa Taifa, Bendera, n.k. na inatafuta uwakilishi kwenye vyombo vya Kikanda, Bara, na Umoja wa Mataifa. Swali ni kwamba ikiwa Muungano ulikuwa ni kati ya Tanganyika na Zanzibar kupata Tanzania, kwa nini ni Tanganyika peke yake imetoweka?

Sura ya kwanza ya katiba imeeleza pia kuwa Jamhuri hiyo ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa yenye kusimamiwa shughuli zake zote za mamlaka ya nchi na vyombo vifuatavyo vikuu:Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Bunge na Baraza la Wawakilishi, katika shuguli hizo kutakuwa na mambo ya muungano na mambo yasiyo ya muungano.

Hivyo basi, kulingana na katiba ya sasa, Tanzania ni nchi isiyo na dini ingawa wananchi wake wana uhuru wa kuchagua dini wazitakazo. Kwa kipindi kirefu kumekuwa na mikutano inayokashifu dini zingine, kutumia Maandiko ya dini zingine katika mahubiri, mjadala wa kuunda Mahakama ya Kadhi, na hata juhudi za kutaka Tanzania iwe mwanachama Umoja wa nchi za Kiislamu (OIC). Mambo haya yanakiuka misingi ya Katiba ya kuwa na uhuru wa kuabudu kwa wananchi wake na nchi kutokuwa na dini. Zaidi ya hayo, historia inaonyesha kuwa wakati nchi inapokuwa na dini ya Taifa, dini hiyo hukandamiza waamini wa dini zingine na kukiuka uhuru wao wa kuchagua imani na kuabudu kwa uhuru.

### HAKI NA WAJIBU MUHIMU

***Haki ya usawa, haki ya kuishi, haki ya uhuru wa mawazo, haki ya kufanya kazi wajibu wa jamii na haki zingine za msingi.***

Pia katiba ya sasa inaainisha haki ya kupata elimu katika vifungu vitatu vya ibara ya 11 kama vifuatavyo;

1. Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanyakazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu, na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi. Na bila kuathiri haki hizo, Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake.

2. Kila mtu anayo haki ya kujielimisha, na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayopenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake.
3. Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vinginevyo vya mafunzo.

Kifungu chenye uhusiano wa namna fulani na menejimenti ya mazingira kiliingizwa kupitia kifungu cha Muswada wa Sheria wa Haki za Binadamu wakati wa marekebisho ya katiba yaliyopitishwa mwaka 1984. Hii imeainishwa kwenye ibara ya 14, inayosema kwamba kila mtu ana haki ya kuishi na ya kupata ulinzi wa maisha yake kutoka kwa jamii. Hiki ni kifungu ambacho Mahakama Kuu ya Tanzania ilikazana kutafsiri katika kutoa hukumu ya haki za kimazingira.

Katika jitihada ya kujaza pengo hili la kikatiba waandishi wa rasimu ya Sheria ya Mazingira[2] (Environmental Management Act – EMA) ya mwaka 2004, waliingiza kifungu kwenye sheria hiyo kinachoainisha "Haki ya Mazingira masafi na yenye afya". Ingawa huu ni ubunifu mzuri, hauna mizizi katika katiba, hivyo kuiacha idara ya mahakama katika hali tatanishi kuhusu misingi ya kisheria ya kifungu hiki ndani ya sheria mama ya nchi (katiba), jambo ambalo wakati mwingine haliwezi kuhakikisha matokeo ya jinsi hakimu binafsi atakavyotafsiri shauri lililoletwa mbele yake. Hii ni kwa sababu mahakama za sheria zinaweza kutoa tafsiri tofauti tofauti kwenye kifungu hiki. Katika hali ambapo kifungu hicho kimeainishwa kwa umakini katika Katiba, hali isingekuwa hivyo. Pia, ni rahisi zaidi kubadilisha kifungu maalum cha sekta ya sheria ambayo inaweza kuathiri haki ya watu kufikia, kuhifadhi na kutunza mazingira. Kwa upande mwingine, siyo rahisi kubadilisha vifungu vya Katiba kuathiri haki ya watu kufikia, kuhifadhi na kutunza mazingira iliyotolewa kwa raia. Hii ni kwa sababu tukio la marudio ya urekebishaji wa katiba mara nyingi huamuliwa na hali ya uhitaji wa haraka kulikoni utaratibu wa kawaida.

Mfumo wa uchumi wa Tanzania ulikuwa wa Ujamaa na Kujitegemea. Baadaye umebadilika na kukosa jina rasmi sasa.

Kutokana na vipengele hivi vya katiba **tunapendekeza** mambo yafuatayo;

- Ili kudumisha Muungano na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali, iwepo Serikali moja tu: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya serikali mbili kama ilivyo sasa au serikali tatu (kwa kurudisha Serikali ya Tanganyika). Jambo ambalo ni muhimu ili kutenda haki kwa nchi zote mbili zilizoungana (Tanganyika na Zanzibar). Tanganyika iongozwe na waziri mkuu na Zanzibar iongozwe na mawaziri kiongozi
- Tanzania iendelee kuwa taifa lisilo na dini na misingi ya uhuru wa kuchagua imani na kuabudu iendelezwe na kulindwa. Serikali isiingilie uhuru wa dini na wala dini yoyote isiingilie uhuru wa serikali. Katiba mpya itamke wazi kuwa kukashifu dini zingine ni kosa la jinai. Serikali

[2] Sheria, Na. 20 ya 2004

isijihusishe katika swala la kuunda mahakama ya kadhi wala kuingiza nchi katika OIC.

- **HAKI ZA KUPATA ELIMU**
    - Katiba mpya itamke wazi kuwa elimu ni miongoni mwa haki za msingi na za lazima kwa kila raia wa Tanzania, tofauti na sasa ambapo inatoa hiyari kwa selikali kufanya au kutofanya jukumu la utoaji elimu kwa raia wake.
    - Katiba mpya iwe na kifungu kinachotamka wazi kuwa uvunjwaji wa "haki ya msingi ya elimu" unaweza kulalamikiwa Mahakamani au katika vyombo vingine halali vya sheria na utoaji haki.
    - Badala ya Katiba kutamka kuwa mwelekeo wetu kama nchi ni wa siasa za ujamaa na kujitegemea, Katiba Mpya itamke kuwa dira yetu ni pamoja na mwelekeo juu ya elimu bora, sayansi na tekinolojia. misingi na meaendeleo ya nchi hii vitalindwa na elimu bora kwanza.
    - Katiba izuie uanzishwaji wa shule, vitengo au taasisi zenye mlengo wa ubaguzi wa kidini, kipato, ukabila, au matumizi ya falsafa ya nchi zingine. Kwa sasa tunaona ongezeko la shule zenye mwelekeo wa Kiasia, Kiingereza, na hata kidini. Taasisi za dini zinazotoa elimu zitofautishe utoaji wa elimu ya kawaida na elimu ya imani zao-imani ya watoto au wazazi wa watoto isiwe kikwazo cha kuzuia wanaotaka kujiunga na shule au taasisi hiyo. Sheria iweke kanuni za kusimamia utoaji wa elimu maalum kwa malezi ya kidini au makundi maalumu kama itakuwa lazima.
    - Ni jukumu la serikali (katika ngazi zote) kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu ya msingi (hadi kidato cha nne-tuondoe ukomo wa darasa la saba kwani kwa mazingira ya sasa kiwango hicho cha elimu hakitoshi, na tayari iwepo wa shule nyingi za sekondari ni maandalizi sahihi yanayoweza kutufikisha huko).
    - Katiba itamke wazi kuwa uanzishaji na ugharamiaji wa elimu ya msingi ni jukumu la serikali za mitaa/miji/majiji pamoja na serikali kuu na sheria itungwe kuhakikisha kuwa wote hawa wanatenga bajeti ya kutosha kutokana na rasimali na hazina iliyopo.
    - Katiba ifafanue kwa undani WAJIBU na HAKI za wadau mbalimbali (wazazi/wananchi, serikali na taasisi zingine) katika kutoa elimu. Kwa utaratibu wa sasa, utoaji wa elimu umekuwa soko la biashara na unahatarisha matokeo ya baadaye.
    - Katiba mpya iwe na kifungu kinachohimiza kuwa, elimu ya awali ni lazima kwa kila mtoto wa Kitanzania, na itolewe kwa usawa mijini na vijijini, sambamba na serikali kuhakikisha kuwa kuna mazingira rafiki kwa wanafunzi wa madarasa ya awali kuweza kujifunza kikamilifu. Katiba ya sasa haitilii maanani suala hili. Katika Sera ya Elimu (2005) Serikali inaonyesha umuhimu wa elimu ya awali, tunanukuu; "Utafiti kadhaa uliofanyika nchini katika miaka ya 1980 ulibaini kuwa watoto waliopitia elimu ya awali huwa na mafanikio makubwa zaidi wanapoanza darasa la kwanza.

**HAKI YA KUPATA HUDUMA YA MAJI SAFI NA SALAMA**

Sera ya Maji ya mwaka 2002 imebaini kuwa maji ni mahitaji na haki muhimu kwa binadamu. Madhumuni na misingi ya Sheria namba 12 ya mwaka 2009 ya Huduma ya maji imelenga katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi wa Tanzania ana haki ya kupata huduma sanifu na endelevu ya maji safi na salama kwa malengo mbalimbali. Pia Tamko la Umojawa Mataifa (UN General Assembly in July 2010) ambapo Tanzania ni Mwanachama na Baraza la Haki za Binadamu Duniani (Human Rights Council in September 2010) imetamka kuwa maji ni haki ya Binadamu ingawa Tanzania imekuwa ikichelewa kusaini tamko hili.

**Water Supply and Sanitation Act (2009): PART 2: Objective and Principles:** The objective of this Act is to promote and ensure the **right** to every person in Tanzania to have the right to efficient, effective, and sustainable water and sanitation services for all purposes

Pia takwimu zinaonyesha kuwa takribani watanzania 26,500 wakiwemo watoto 18,500 walio na umri chini ya miaka 5 hufariki kila mwaka kutokana na magonjwa ya kuhara ambayo takribani asilimia 90% inachangiwa na ukosefu wa maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira na afya siha. [3]Hii inakiuka haki ya msingi ya binadamu ya kuishi. Pia Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 49.7% tu ya watanzania waishio vijijini ndio wanaopata huduma ya maji safi na salama kulinganisha na asilimia 80% ya wale waishio mijini Takwimu hizi zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya watu waishio vijiji hawapati huduma ya maji safi na salama ingawa idadi kubwa ya watu wanatoka vijijini. Hii ni kinyume na haki ya usawa kama ambavyo ilivyo katika katiba ya sasa Sura ya Kwanza Sehemu ya Tatu ibara namba 12 (Usawa wa binadamu)

Kwa kuzingati maelezo hapo juu pamoja na kipengele kilichopo kwenye katiba ya sasa, Sura ya Kwanza Sehemu ya tatu ibara ya 14 (Haki ya Kuwa hai) na kile kilichopo Sura ya Kwanza Sehemu ya Tatu ibara namba 12(Usawa wa binadamu)

Tunapendekeza katiba mpya izingatie yafuatayo ;

- Katiba mpya itamke kuwa maji ni haki ya msingi ya kila mtanzania

- Haki na Uhuru wa upatikanaji wa maji – Uhuru huu unahusisha: kukatiwa huduma ya maji bila taarifa kinyume cha sheria, kinga ya kisheria ya kuchafua vyanzo vya maji na ubaguzi katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama)
- katiba itamke upatikanaji wa kima cha chini wa maji safi na salama ya kunywa kuendeleza uhai na kulinda afya (Katiba mpya itamke kuwepo na usawa katika upatikanaji wa huduma ya maji bila kuzingatia eneo mtu anakotoka, kundi fulani, Jinsia, wala rika, Katiba itamke kuwa upatikanaji wa maji uwe katika uwezo ambao kila mtanzania anaweza kumudu)

[3] Water and Sanitation Program(2012): Economic Impacts of poor Sanitation in Africa

- Katiba itamke wajibu wa jamhuri kujizuia kuingilia moja kwa moja au njia nyingine yoyote juu ya matumizi ya Maji - (Katiba itamke kuwa upatikanaji wa maji uzingatie misingi endelevu, usawa na uwajibikaji kwa mamlaka husika)

- Katiba itamke kuwa dola itengeneze vyombo husika vitakavyosimamia, sera, rasilimali, sheria, utawala sahihi ili kutimiza na kutambua upatikanaji wa haki ya Maji. (kuwa, ukiukwaji wa haki ya upatikanaji wa huduma ya maji unaweza kulalamikiwa makahamani au kwenye vyombo vingine vya sheria)

- **UHURU WA KUPATA HABARI, HAKI NA UHURU WA MAWAZO**
  Katika iliyo katiba ya sasa ibara ya 18 kifungu (a) mpaka (d) kinaelezea juu ya uhuru na haki ya mtu kutoa mawazo na maoni yake pamoja na kupata habari/taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali.

  Kwa kuzingatia ibara hiyo na ili kuongeza uwazi na uwajibikaji wa serikali kwa wananchi katika utoaji huduma kwa kuzingatia misingi ya haki tunapendekeza;
  - Katiba itambue kwamba kuheshimika kwa uhuru wa kujieleza sambamba na haki ya kupata taarifa vikiwemo ndani ya taasisi za umma na taasisi nyingine, itasababisha kuwepo kwa serikali yenye uwazi na uwajibikaji kwa umma, pamoja na utawala bora na kuimarika kwa demokrasia
  - Katiba mpya iweze kujumuisha kipengele cha IV kilichopo katika Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu- Azimio la Misingi ya Uhuru wa Kujieleza- Afrika, 2002 kinachosema;
    - 1. Taasisi za umma zina dhamana ya kuhifadhi taarifa lakini si kwa matumizi yao tu bali kama waangalizi/ wasimamizi wa mali za umma na kila mtu ana haki ya kupata taarifa hizo kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo kisheria.
    - Haki ya kupata taarifa itahakikishwa na sheria kwa kuzingatia misingi ifuatayo:
      - Kila mtu ana haki ya kupata taarifa zinazohifadhiwa na taasisi za umma
      - Kila mtu ana haki ya kupata taarifa zinazohifadhiwa na taasisi binafsi, taarifa ambazo ni muhimu katika kulinda haki yoyote:
      - Zuio lolote la kutoa taarifa litakatiwa shauri au kupelekwa mahakamani;
      - Taasisi za umma zitatakiwa, hata bila ya kuwepo maombi yoyote, kuchapisha taarifa ambazo ni muhimu kwa maslahi ya umma:
      - Hakuna mtu yeyote atakayezuiwa kutoa taarifa zenye nia njema ya kufichua maovu , au tishio kwa afya, usalama au mazingira isipokuwa pale ambapo zuio hilo litawekwa ili kulinda maslahi na demokrasia ya jamii husika.

- Sheria za Usiri lazima zirekebishwe ili kuendana na misingi ya haki ya kupata taarifa

- **USAWA WA KIJINSIA**
  - Katiba itamke wazi kuwa serikali itawajibika kuchukua hatua za kutunga sharia ambazo zitahakikisha usawa wa kijinsia katika Nyanja mbalimbali nchini ikiwemo ajira na umiliki wa ardhi, pamoja na urithi wa mali.
  - Katiba itamke wazi kuwa bila kujali jinsia, mwananchi atahakikishiwa haki ya kupata msaada wa kisheria kwenye masuala yote yanayohusisha uhusiano wake na michakato ya mahakama. Maamuzi ya mahakama pia yazingatie usawa wa kijinsia. Katiba pia itamke kuwa mahakama inapotoa maamuzi yanayomathiri mwananchi, awe mwanamke au mwanaume, lazima itoe maelezo ya hukumu yake kwa maandishi na imwelekeze mhusika mikondo/njia mbadala za kufuata kama atataka kukata rufaa.

- **NDOA**
  - Katiba itamke kuwa kila mtu ana hiari ya kuoa au kuolewa na ndoa ni muunganiko wa hiari wa mwanamke na mwamanume wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

- **HIFADHI YA JAMII**
  - Katiba itamke kuwepo kwa haki ya hifadhi ya jamii kwa watu wote yakiwemo makundi maalum

# SURA YA PILI

# SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

Serikali ya Jamhuri ya Muungano inayo mamlaka juu ya mambo yote ya muungano katika Jamhuri ya muungano na pia juu ya mambo mengine yote yahusiyo Tanzania bara. Muundo wa serikali hiyo ni Rais,Makamu wa Rais,Waziri Mkuu,Baraza la Mawaziri na Serikali.

Katika ibara ya 39(1)(c) na ibara ndogo ya (2) ambayo inatoa sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Rais, sifa mojawapo ni kuwa ni lazima mtu huyo awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa.

Ibara ya 41(6) ya katiba ya sasa inaeleza kuwa mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo tu amepata kura nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yeyote.

Katiba ya sasa imetoa utaratibu wa kumchagua Rais ambapo ibara ya 41 (7) inaeleza wazi kuwa iwapo mgombea ametangazwa na tume ya uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa ibara hii, basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

Pia katika ibara ya 42(1) inaeleza kuwa Rais mteule atashika madaraka ya Rais mapema iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwamba amechaguliwa kuwa Rais, lakini kwa hali yoyote itabidi ashike madaraka kabla ya kupita siku saba.

Ibara ya 46(3) inatoa kinga ya Rais dhidi ya mashtaka ya madai ambapo inaelezwa wazi kuwa isipokuwa kama ataacha kushika madaraka ya Rais ni marufuku kumshtaki Rais au kufungua mahakamani shauri lolote la jinai au la kumdai mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Rais baada ya kuacha madaraka hayo kutokana na jambo lolote alilolifanya yeye kama Rais wakati alipokuwa bado anashika madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba. . Kinga hii inatoa mianya ya uwezekano wa kutumiwa vibaya katika maswala ya kukiuka haki za binadamu na uvunjaji wa sheria.

Kwa sasa, Rais ndiye mwenye madaraka ya kuteua Waziri Mkuu; Mawaziri wote na Manaibu wao; Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa; Mkuu wa Majeshi; Wakuu wa Majeshi Mbalimbali; Makatibu wakuu wa Wizara; Wakurugenzi wa Wizara, Taasisi, na Idara zote; wakuu wa Vyuo Vikuu vyote vya Umma; Wakuu wa Mikoa; Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji; anaunda Wizara, Tume, Mikoa, na Wilaya Mpya; n.k. Madaraka haya ni makubwa mno na yana athari kubwa katika kuendeleza utawala bora na kujenga uhuru na uwezo wa kutoa maamuzi yenye utashi wa dhati kwa watendaji wanaoteuliwa.

Katika ibara ya 51 (2) ya katiba inaeleza uchaguzi wa Waziri Mkuu, ambaye anatakiwa kuteuliwa na Rais baada tu ya siku kumi ya kushika madaraka yake na atatoka katika jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye wabunge wengi bungeni au kama hakuna chama cha siasa chenye wabunge wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na wabunge walio wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na wabunge walio wengi kuwa waziri mkuu wa Jamhuri ya muungano, naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za wabunge walio wengi.

Katika Katiba ya sasa inatoa jinsi ambavyo uteuzi wa mawaziri unatakiwa kufanyika katika ibara ya 55, ibara ya 55(4) inasema “Mawaziri na Naibu Mawaziri wote watateuliwa kutoka miongoni mwa wabunge”.

**Tunapendekeza** vitu vifuatavyo viwepo ili viweze kuiboresha serikali ya Jamhuri ya muungano;

- Katiba mpya iruhusu nafasi za wagombea binafsi katika chaguzi mbalimbali za uongozi wa nchi.
- Kuwe na Tume huru ya Uchaguzi. Muundo wa tume huru:
    - Wajumbe wa tume ya uchaguzi wateuliwe kutokana na mapendekezo ya jumuiko la vyama vyote vya siasa nchini (all-party congress) na kuridhiwa na Bunge. Jumuiko hilo la vyama litajumuisha viongozi wawili wakuu kutoka kila chama na kuratibiwa na katibu ambaye atateuliwa na wajumbe wa tume yenyewe hivyo kuwajibika kwao.
    - Ripoti zote kuhusiana na mwenendo wa chaguzi nchini zitapitishwa na Bunge.
    - Matokeo ya chaguzi za wabunge yatangazwe ndani ya saa 24 baada ya uchaguzi
    - Matokeo ya Uchaguzi wa Rais yatangazwe ndani ya saa 72 na Rais aapishwe baada ya siku 30 au 60 ili kutoa nafasi ya kuthibitisha matokeo na kupinga matokeo ya Rais mahakamani. Ikiwa Mshindi atatuhumiwa na

kuthibitishwa na Mahakama kwamba ametumia rushwa basi asiruhusiwe kugombea nafasi yoyote ya uongozi wakati wowote.
    - Wakati wa kampeni Rais akiwa miongoni mwa wagombea akabidhi ofisi kwa mtu atakaye bainishwa na katiba ili aweze kushiriki kampeni za urais bila ya kutumia kofia ya urais.
    - Katiba itamke wazi kuwa rais atapatikana kwa ushindi wa kura zaidi ya asilimia 51 na kuendelea.
    - Katiba itamke wazi kuwa, pale ambapo hakuna mgombea urais aliyefikisha asilimia 51 ya kura zote, mshindi wa kwanza na wa pili wataunda serikali ya umoja iwapo jumla ya kura zao zinafikia asilimia 51 au zaidi ya kura zote. Vinginevyo itabidi uchaguzi urudiwe kwa mshindi wa kwanza hadi wa tatu

- Ili kutoa uhuru wa rais kutekeleza madaraka yale ipasavyo bila kuingiliwa na chama, katiba itamke wazi kuwa, rais hatapoteza urais wake kwa kukihama chama. Yaani, Rais anaweza kuhama chama alichopatia u-rais na bado ataendelea kuwa Rais wa nchi.
- Katiba itamke wazi kuwa, Rais anaweza kushtakiwa baada ya kumaliza mda wake endapo itaonekana kuwa alitumia madaraka yake vibaya
- Rais awe na madaraka ya kumteua Waziri Mkuu, Jaji Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Polisi (IGP), na Mkuu wa Usalama wa Taifa na uteuzi wa kila mmoja wa hao uthibitishwe na Bunge kwa kura za siri kwa walau theluthi mbili (66.67%)
- Kusiwepo na cheo cha Makamu wa Rais. Rais akifa, basi Jaji Mkuu, Waziri Mkuu, au Spika wa Bunge ashike nafasi ya Rais kwa siku 90 kisha Rais mpya achaguliwe.
- Waziri Mkuu ateue Mawaziri na Jaji Mkuu ateue Majaji ambao nao watathibitishwa na Bunge kwa kura za siri kwa walau theluthi mbili (66.67%) isipokuwa mkuu wa usalama wa taifa na mkuu wa majeshi ya ulinzi na usalama (JWTZ).
- Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Wakurugenzi waombe kazi na kuajiriwa kitaaluma kwenye Tume Huru ya Utumishi. Maombi yao yachambuliwe na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kisha majina yao yapelekwe kwa Waziri Mkuu kusubiri uchaguzi wa Wabunge kukamilika na Bunge kuundwa. Kama yeyote kati yao atakuwa amegombea Ubunge na kuchaguliwa, jina lake litaondolewa kwenye maombi ya kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waziri, Katibu Mkuu, au Mkurugenzi. Nafasi yake ijazwe na waombaji wengine. Baada ya Bunge kuundwa, waziri mkuu atafanya uteuzi wake kutokana na walioomba nafasi hizo.
- Waziri mkuu atawasilisha katika Bunge orodha ya aliowateua kushika nafasi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, mawaziri na Wakurugenzi ili wathibitishwe na Bunge kwa kwa kura za siri kwa walau theluthi mbili (66.67%)
- Idadi ya Wizara isizidi kumi na tano (15) na kila waziri, atakuwa na naibu mmoja tu.
- Maeneo maalum kwa ajili ya kinga kwa viongozi yaanishwe ili kupunguza uwezekano wa mtu yeyote kuwa juu ya sheria. Kwa mfano, kinga isimlinde Kiongozi kwa vitendo vya kukiuka haki za binadamu kama vile kuoana na mke wa mtu au kuolewa na mume wa mtu mwingine, kupeleka nchi vitani kinyemela, kukiuka Katiba, kuhujumu uchumi, kufanya kitendo chochote kinachohujumu maendeleo ya nchi kwa miaka ya mbeleni kama kuingia mikataba feki.
- Iwe ni marufuku kwa kiongozi yeyote wa umma kutumia rasilimali za umma katika shughuli za chama cha siasa.

# SURA YA TATU

# BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

Bunge la Jamhuri ya Muungano ni chombo muhimu sana chenye maamlaka ya kufanya maamuzi ya nchi na kutengeneza sheria na linahusisha Rais na Wabunge.
Katiba ya sasa katika ibara ya 66 (1) inaainisha aina za wabunge ambao ni wabunge waliochaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi, wabunge wa viti maalum, wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais,Spika. Wabunge watano waliochaguliwa na baraza la wawakilishi, mwanasheria mkuu.

Wagombea ubunge kwa mujibu wa ibara ya 67(1)(a) wanatakiwa kujua kusoma na kuandika tu ingawa majukumu ya Bunge ni makubwa na yanahitaji uwezo mkubwa wa kuchambua mambo mbalimbali yanayohusu uchumi, jamii, sheria, takwimu, siasa, elimu, na taaluma mbalimbali kwa upeo wa hali ya juu ili kushiriki kikamilifu katika shughuli za kutunga sheria na kuisimamia serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Katika ibara ya 84(1) ya katiba ya sasa inaelezea uchaguzi wa spika wa bunge ambaye huchaguliwa na wabunge kutoka miongoni mwa watu ambao ni wabunge au wenye sifa za kuwa mbunge:atakuwa ndiye kiongozi wa bunge na atawakilisha bunge katika vyombo na vikao vingine vyote nje ya bunge.

Kwa mujibu wa ibara ya 74 (1) ya katiba ya sasa Rais ndiye mwenye mamlaka ya kuteuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.
Usimamizi wa Bunge uliohuru unahitaji pawepo na uhalisia wa kutenganisha na kuwa na uwiano mzuri wa mamlaka kati ya Bunge na Serikali. Pale ambapo hakuna mipaka na serikali ikiwa na nguvu kubwa kuliko bunge katika utoaji habari na rasilimali, achilia mbali kamati za usimamizi, haiwezekani
kwa bunge kuwa na uwezo wa kuwa na makali endelevu dhidi ya serikali. Kwa kuangalia utendaji wa Usimamizi wa Bajeti ya Bunge katika mazingira haya, hoja ya umuhimu wa kuanzisha Ofisi ya Bajeti ya Bunge inaweza kuibuliwa

Kulingana na hivi vipengele vya katiba ya sasa **tunashauri** yafwatayo yafanyike ili kuweza kuboresha kazi za bunge la Jamhuri ya Muungano;

- Kiwango cha chini cha elimu kwa wabunge kiwe shahada ya kwanzaWawepo Wabunge wa Majimbo tu
- Idadi ya majimbo ilingane na idadi ya Wilaya – yaani Jimbo moja kwa kila Wilaya
- Spika wa Bunge asiwe mbunge na asitokane na chama chochote cha siasa. Awe Mtaalamu na aombe nafasi hiyo kupitia Idara ya Utumishi wa Umma kama watakavyoomba mawaziri.
- Maamuzi yote muhimu yawe kwa kura za siri zitakazoonyeshwa wazi baada ya kupigwa badala ya kusema NDIYO au HAPANA tu
- Utendaji wa Wabunge utathminiwe kila mwaka ili kuona kama wanatekeleza wajibu wao ipasavyo hii itatoa fursa kwa wananchi kumwajibisha mbunge wao.
- Chama chochote kisiwe na mamlaka ya kumvua ubunge mwanachama wake kwa vile mbunge anachaguliwa na wananchi wa jimbo lake kutoka chama chake na wasiotoka katika chama chake.
- Kiwango cha kulipwa posho wabunge kiendane na mapato na hali ya uchumi kwa kuzingatia ongezeko sawa la mishahara kati ya wafanyakazi wengine wa serikali

na wabunge. Pia viwango vya kulipwa wabunge viinua mgongo vipunguzwe kwa kuzingatia ulinganifu na watumishi wengine wa serikali.

- Iwapo mbunge/waziri atahusika katika skendo fulani au kushindwa kufanya vizuri katika wizara/ wajibu zake, awajibishwe katika kosa hilo bila kuficha na wasipate tena nafasi ya kuhamishiwa vitengo vingine.
- Muundo wa bunge uwe pia katika sehemu tatu, yaani bunge la Jamhuri, bunge la Tanganyika na lile la Zanzibar ili kutoa vipaumbele vya kila nchi katika kujadili mambo yao kwa uhuru.
- Chaguzi za wabunge zisirudiwe endapo taratibu zilikiukwa badala yake anayefuata kwa kura apewe nafasi hiyo. Kama ubunge wa mbunge umetenguliwa kwa sababu alikiuka sheria kwa kutoa rushwa au vinginevyo na mahakama imethibitisha, asigombee tena mpaka ipite miaka 10
- Kuwe na ukomo wa Ubunge. Wabunge wasiruhusiwe kuwa wabunge kwa zaidi ya vipindi viwili vya uwakirishi.
- Kulingana na majukumu makubwa waliyonayo wabunge tunapendekeza katiba mpya itambue uwepo wa ofisi ya bajeti ya bunge itayokuwa inafanya uchambuzi wa bajeti ya taifa kiutalaam.

# SURA TANO

## UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO, MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO, TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA YA TANZANIA BARA,MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR,MAHAKAMA YA RUFANI YA JAMHURI YA MUUNGANO NA MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO.

Mahakama ya Tanzania imo ndani ya wizara ya sheria na mambo ya katiba. Hii inaifanya kuwa sehemu ya dola na uhuru wake unaingiliwa kirahisi hata katika kesi mbalimbali zilizoamriwa kama ile ya rufaa ya serikali dhidi ya mchungaji Christopher Mtikila kwenye shauri la mgombea Binafsi ambapo katiba iko wazi kwa upande mmoja na upande mwingine unamnyanganya haki kwa kumlazimisha ajiunge na chama cha siasa ili aweze kugombea ubunge au Urais.

**Tunapendekeza** yafuatayo:-

- Mahakama iwe huru, iendolewe katika wizara ya sheria na mambo ya katiba, iwe kama vile Bunge. Rais atateua jaji mkuu na jaji mkuu atateua majaji wengine (kwa kushirikiana na kamati maalum ya majaji wastaafu na wale maamuzi yao yalizingatia haki za binadamu katika muda wote wa utumishi wao) na kuwaapisha kutumika kama jaji.

# SURA YA SITA

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA NA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA.**

Ni muhimu viongozi wanaowakilisha wananchi wawe na maadili mema hivyo basi katika katiba ya sasa kuna sekretariti ya viongozi wa umma inaoshughulikia hili pia, kuna tume ya haki za binadamu na utawala bora ambayo inajikita na ukiukwaji wa haki za binadamu.

**Tunapendekeza** kwamba,

- Tume ya haki za Binadamu na utawala bora, (sura ya 129-131 ya katiba ya sasa) ipewe nguvu ya kuchunguza hata hakuna malalamiko yaliyoletwa mbele yake ili mradi wanatetea haki za binadamu. Ibara ya 131 (2) (c na d) inaonyesha wazi kuwa tume hii ya haki za binadamu haitakiwi kuchunguza jambo lolote lihusilo madaraka ya Rais kutoa msamaha au jambo jimgine lililotajwa na sharia yoyote hivyo basi vipengele hivi zifutwe kwa sababu zinamweka Rais juu ya sheria.
- Katiba iweke vizuri namna ya kushughulikia kero za wananchi zinazowalazimisha wananchi kuingia katika maandano na migomo.

- Suala la uwajibikaji liwe la kikatiba. Katiba iweke wazi utaratibu wa kumwajibisha kiongozi wa kuchaguliwa anapokuwa hawawakilishi wananchi wake

## SURA YA SABA

## MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

Ibara ya 143(4) ya katiba ya sasa inasema wazi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa, baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusikawawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza hicho kikao.

Tunashauri yafuatayo yawekwe ili kuboresha masharti yahusiyo fedha ya Jamhuri ya Muungano;

- Taarifa za ukaguzi za CAG zipelekwe kwa Rais kwa taarifa, nakala zipelekwe kwa DPP kufungua mashtaka kwa wote waliohusika na upotevu wa mali za umma.
- Ripoti ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) iwe na tathmini ya utekelezaji wake kila baada mwaka mmoja ili kuona jinsi maazimio yanavyotekelezwa. Mkuu wa Mashtaka (DPP) atoe taarifa Bungeni kila mwaka kabla ya ripoti mpya ya ukaguzi. Wale wote ambao hawatakuwa wametekeleza, wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Public Service Act au njia nyingine inayotajwa na katiba hii na taarifa iwasilishwe bungeni katika kikao kinachofuata.

- Bunge lihusike moja kwa moja katika kupitia mikataba yote na kuipitisha au kuibatilisha ili kuzuia taifa kupata hasara kwa sababu ya mikataba mibovu na isiyo na manufaa isipokuwa kwa wachache. Iwapo mkataba wowote utafanyika kinyume na hapo utabainika kuwa batili kitaifa na kimataifa na hakutakuwa na fidia yoyote katika kukatisha mkataba huo.

## SURA YA NANE

## MADARAKA YA UMMA

Muundo wa Serikali za Mitaa umeainishwa katika sehemu ya tatu ya Sheria za Serikali za Mitaa ya 7 na 8 ya mwaka 1982. Sheria hizi zimeainisha kwamba, Serikali za Mitaa zinaundwa na Halmashauri ya Wilaya, Mamlaka za Miji na Vyombo vya Serikali za Vijiji. Katika muundo huu wa serikali za mitaa, baadhi ya vyombo vinavyounda serikali hii vinaongozwa na wenyeviti wanaochaguliwa miongoni mwa wanajamii wa eneo husika mfano Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji.

Ila ikumbukwe kwamba kwa sehemu kubwa Rais anayo madaraka ya kuteua watendaji wakuu katika Serikali Kuu. Mfano Rais ana mamlaka ya kuwateua Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kama ilivyoainishwa katika ibara ya 61(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makatibu.

Tawala wa Wilaya na Mikoa. Kwa mantiki hiyo basi, mamlaka haya makubwa aliyonayo Rais yanaminya uhuru wa Serikali za Mitaa katika utendaji wake wa kazi. Hii ni kwa sababu serikali hizi za mitaa kama ilivyo kwa watumishi wengine wa serikali,inafanya shughuli zake kwa niaba ya serikali na kwa amri na maagizo yatakayothibitishwa kwa namna itakavyoelezwa katika kanuni zilizowekwa na Rais kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya 35(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ibara ya 35(2) na 36(4) inampa Rais mamlaka ya kuteua na kuwawajibisha watendaji wa serikali.

Kutokana na mamlaka aliyopewa Rais kwenye ibara ya 35(1), (2) na 36(4) kuna uwezekano mkubwa kwa viongozi ambao kimsingi ni wateule wa Rais kufanya kazi kwa malengo ya kukidhi matakwa ya Rais na si kwa ajili ya wananchi.

Ili kuepuka mapungufu hayo, Rais asiwe na mamlaka ya kuwateua na kuwawajibisha watendaji katika serikali za mitaa, badala yake wawe wanachaguliwa na wananchi katika mikoa na wilaya husika. Hii itasaidia kuondoa ukiritimba katika utendaji kazi wa serikali za mitaa na kuongeza ufanisi kwani watendaji katika serikali za mitaa watafanya kazi kwa moyo kutokana na uzoefu wa maeneo hayo na ufahamu wa matakwa ya wadau kwa kuwa ni makazi yao ya muda mrefu.

Serikali za mitaa ziwe na muundo wake wa uongozi na utendaji tofauti na serikali kuu. Ikiwezekana kuwe hata na mwakilishi kutoka katika serikali za mitaa bungeni kama ilivyo kwa wabunge katika serikali za mitaa wanapokuwa wajumbe wa baraza la madiwani. Hii itasaidia kuboresha utendaji kazi wa serikali za mitaa kwa faida ya umma na kuboresha mahusiano ya kikazi baina ya serikali kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na serikali za mitaa.

Nchi mbalimbali zimeandaa katiba ambayo imeweka majukumu na kutoa madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa. Mfano mzuri ni Katiba ya Kenya ya mwaka 2011 ambapo ibara ya 6 inasema serikali itakuwa na ngazi kuu mbili yaani Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Ibara ya 174 ya katiba ya Kenya inazungumzia kwa ufasaha zaidi juu ya umuhimu wa ugatuzi (devolution) wa Madaraka kutoka Serikali Kuu hadi Serikali za Mitaa ukilenga kutekeleza na kuimarisha mambo yafuatayo:

a) Kuimarisha demokrasia
b) Kuwapa wananchi madaraka zaidi ya kujitawala na kujiamulia
mambo yao wenyewe kwa manufaa ya eneo lao
c) Kuwapa wananchi mamlaka zaidi ya kujitawala wenyewe (selfgovernance),
ushirikishwaji na kudumisha demokrasia
d) Kutambua haki ya jamii ya kusimamia mambo yao wenyewe
e) Kulinda haki za watu wachache (minorities)
f) Kuimarisha uwiano katika kutumia rasilimali
g) Kuimarisha utoaji wa huduma za jamii katika ngazi ya chini
h) Kuimarisha dhana ya kusimamiana (checks and balance) na
mgawanyo wa madaraka (separation of powers)
i) Kuimarisha dhana ya usawa wa kijinsia katika ngazi za chini.

Ibara ya 6 na ya 151 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa maana ya neno "Serikali" na kutambua uwepo wa Serikali za Mitaa kimuundo na kimajukumu. Katiba inaeleza madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa kuwa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. (ibara ya 146). Msingi wa azma ya kupeleka madaraka kwa wananchi ni kukidhi haja ya kikatiba ya ibara ya 8 inayosema:

"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo (a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi na kwa mujibu wa katiba hii; (b) lengo kuu la serikali litakuwa ustawi wa wananchi (c) serikali itawajibika kwa wananchi na (d) wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya katiba hii"

Pamoja na katiba kueleleza muundo na kazi za serikali za mitaa ( ibara ya 145 na 146) na nguvu ya wananchi kufafanuliwa vema (ibara ya 8), serikali hizi zimebaki na uhuru finyu wa kujiamulia na kutekeleza mambo yake ukilinganisha na serikali nyingine na hatimaye kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Kwa mujibu wa ibara ya 146(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania serikali za mitaa zitakuwa na majukumu yafuatayo:

1. Kutekeleza kazi za serikali za mitaa katika eneo lake
2. Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi
3. Kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kuitumia demokrasia
4. Kuharakisha maendeleo ya wananchi.
5. Majukumu mengine ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria ni kama ifuatavyo:
6. Kudumisha amani, usalama na utulivu katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa,
7. Kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa wakazi wake,
8. Kutekeleza shughuli za maendeleo yanayolenga katika kuboresha,huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa,
9. Kupanga mipango ya maendeleo endelevu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa zinazozingatia mipango ya maendeleo vijijini na mijini,
10. Kuchukua hatua madhubuti za kulinda na kuendeleza hifadhi ya mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa,
11. Kuendeleza sera ya serikali ya upelekaji wa madaraka kwa umma yanayohusu maeneo ya siasa, fedha na utawala katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa,
12. Kuimarisha ushiriki wa wananchi kwa lengo la kuimarisha demokrasia katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa,
13. Kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha vilivyopo katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Hapa tunachambua nafasi na mamlaka ya serikali za mitaa na kueleza mapungufu ya kiutekelezaji kwenye maeneo ya maamuzi, kuweka mipango, kutekeleza majukumu na kufanya tathmini au kupima mafanikio.

Kutokana na changamoto mbalimbali zinazokabili utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Katiba itoe mwongozo juu ya namna wananchi watakavyoshiriki katika maamuzi na pia katika shughuli za maendeleo, uchumi wa nchi, huduma za jamii na maisha yao kwa ujumla. Hii itawezesha kuziimarisha na kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi katika ngazi za chini. Katiba itoe mwongozo juu ya kuanzishwa na kutekelezwa kwa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ulioanza mwaka 1998 ambao ulilenga katika kupeleka madaraka kwa wananchi.

Katiba ilenge katika kutekeleza dhana ya Upelekaji wa Madaraka kwa wananchi kama ilivyoelezwa kwa kina zaidi katika Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1998. Katika Sera hii, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapewa uhuru

wa kufanya maamuzi mbalimbali yahusuyo utoaji wa huduma kwa wananchi walio katika Mamlaka zao.

Kwa ujumla hapa Tanzania kumekuwepo na juhudi mbalimbali za kupeleka madaraka kwa wananchi. Juhudi hizo ni kama vile madaraka mikoani na maboresho ya serikali za mitaa. Hata hivyo, kuna udhaifu katika aina hii ya uwezeshaji kwani mara nyingi kinachotokea ni mategemeo kuwa serikali itawawezesha wananchi. Lakini imekuwa ikichukua muda mrefu kwa Serikali Kuu kupunguza mamlaka yake kirahisi. Mara nyingi badala ya mamlaka zaidi kupelekwa kwa wananchi, kinachotokea huwa ni Serikali Kuu kutaka kuongeza udhibiti.

Pamoja kuwepo kwa sheria zingine, Katiba inatakiwa iangalie kwa ufasaha dhana hii ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa.

Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa wakati huu ambapo serikali imejitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa uchumi, kinachotokea ni uwezeshaji wa aina fulani pale ambapo serikali inaingia ubia au kuruhusu asasi za kiraia kujihusisha na maeneo kama utunzaji wa mazingira, ulinzi na usalama,mapambano dhidi ya rushwa, utoaji wa huduma za jamii, nk.

Moja kati ya shughuli kuu za Serikali za Mitaa ni kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kutumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi (ibara 146).

Hata hivyo kwa mujibu wa sheria ya Serikali za Mitaa (toleo la 2000) ,maamuzi ya kanuni na miongozo ya uendeshaji wake yanategemea kibali cha waziri anayehusika na Serikali za Mitaa. Hii ni ishara kwamba halmashauri zetu haziwezi kusonga mbele kimaamuzi bila kibali cha waziri ambae kimsingi ni mtumishi wa serikali kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Wakati Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji zikipewa nafasi finyu ya kujiamulia mambo yao, wananchi walio ndani ya halmashauri hawana sheria inayowasaidia kuwabana viongozi na watendaji wao kuwajibika moja kwa moja kwa wananchi hasa wanapokuwa wamefanya maamuzi ambayo sio kipaumbele cha wananchi.

Kipindi hiki tunapoandika katiba mpya kuna haja ya kufikiria uhuru na kujitegemea kwa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Vijiji.

Mjadala unafaa kujielekeza kwenye utafutaji wa njia mbadala ya kufanya serikali kuu kuwa mshirika mwenza wa serikali za mitaa ili kufanya kazi kwa pamoja ki-ushirikiano zaidi badala ya serikali kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) kuwa mwongozaji wa maamuzi ya serikali za mitaa.

Kutokana na uzoefu wa serikali kupata hasara kupitia mikataba mibovu serikali inayoingia na wawekezaji, ingefaa mikataba yote inayoingiwa baina ya serikali na wawekezaji ijadiliwe na kuridhiwa na bunge na viongozi wa Serikali za Mitaa katika maeneo ambayo miradi hiyo itatekelezwa. Hii itaisadia serikali kuingia katika mikataba ambayo itakuwa na manufaa kwa umma kwani Serikali za Mitaa ambazo ndizo zinazofanya kazi moja kwa moja katika jamii zitashirikishwa katika kutoa maamuzi.

Katika zama hizi za kidemokrasia, mtindo mzuri wa kuongoza watu ni kuwashirikisha katika mipango na utekelezaji wa majukumu ya umma.

Katika jamii ambazo zimeonesha kufanikiwa kimaendeleo, pana ushahidi wa kutosha kwamba mchango wa kila mwananchi ama kupitia vikundi vyao umeonekana hasa pale waliposhirikishwa kwenye kupanga na kutekeleza.

Hili litawezekana tu pale ambapo ‘vyombo vya serikali za mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote’ (ibara ya 146) .

Pamoja na ubunifu wa serikali kuwa na sera iliyopelekea Mchakato wa Kuibua Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD), hapajawekwa sharia inayowabana wanamipango na viongozi kuwajibika endapo vijiji na mitaa hawakushirikishwa kwenye zoezi la kuweka mipango kwa kukubaliana vipaumbele.

Uzoefu unaonesha pia kwamba pamoja za zoezi la O&OD kuanzia ngazi ya chini na bajeti za awali kuwekwa na Halmashauri za Wilaya, Manisapaa na Miji, Serikali Kuu bado inahodhi maamuzi ya shughuli zipi zifanyike. Hii imepelekea kila mara halmashauri zetu kujikita kwenye miradi ambayo si kipaumbele cha wananchi ilimradi tu kwamba wapate pesa kuendesha halmashauri. Kinadharia bado kuna ushiriki finyu wa wananchi katika kuandaa mipango.

Katiba mpya iweke utaratibu utakaowalazimisha viongozi wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) kuheshimu maamuzi ya vikao halali vya Serikali za Mitaa vilivyoainisha vipaumbele vya wananchi, na hivyo ndivyo vitengewe fedha/rasilimali na si kuwabadilishia. Pamoja na hilo, Katiba mpya iweke misingi ya uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi ikiwemo ulazima wa kuwashirikisha kwenye kupanga na kutekeleza shughuli za Serikali za Mitaa.

Ni utamaduni wa kawaida kuona kwamba kama watu walifanya maamuzi ya pamoja, wakashirikiana kutekeleza inapendeza na tena ni muhimu watu hao wakawa pamoja kwenye kutathmini na kupima mafanikio. Jambo hili likifanyika kwa dhati na kwa moyo mweupe huepusha minong’ono na huifanya mamlaka husika kuaminika zaidi kwa wananchi na kuwavutia wajitolee nguvu na rasilimali zao tena kwenye mipango ya badae.

Moja ya misingi ya demokrasia hasa ngazi ya jamii ni ushiriki wa wananchi kwenye mchakato mzima wa maendeleo ikiwemo hatua ya kufuatilia na kutathmini mafanikio. Madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Kwahiyo vyombo vya serikali za mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla kama ilivyoelezwa katika ibara ya 146 (1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Eneo hili limekuwa likipuuzwa mara nyingi kwa sababu ya mianya iliachwa ndani ya katiba iliyopo kwani katiba inaonesha namna ya kufanya maamuzi ngazi ya halmashauri kwenye Mikutano Mikuu ya Kijiji bila kuonesha kuwa wananchi wanapata muda upi kuhoji matunda ya ushiriki wao kwenye hatua zote za awali.

Mapendekezo yetu ni kwamba tuweze kujikita kuweka mfumo ambao utawaleta viongozi karibu na wananchi ili waweze kujisikia kuwajibika hata hatua za mwisho za ufanisi au kushindikana kwa miradi ya umma.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 145(2) bunge au baraza la wawakilishi, kadri itakavyokuwa, litatunga sharia itakayofafanua

utaratibu wa kuanzisha vyombo vya Serikali za Mitaa, miundo na wajumbe wake, njia za mapato na utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo.

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (The Local Government Finances Act, 1982) imeainisha vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri za Wilaya Na Vijiji.

Serikali za Mitaa zinapata mapato yake kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivi ni pamoja na fedha zitokanazo na biashara, viwanda, huduma, ada ya leseni, ushuru, vibali, nk. Baadhi ya makusanyo ya mapato katika Serikali za Mitaa yanafanywa na taasisi za Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Pamoja na kwamba fedha hizi zinakusanywa kutoka kwenye Serikali za Mitaa, matumizi yake yanaamuliwa na Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania). Makusanyo ya serikali za mitaa hubaki serikali za mitaa isipokuwa makusanyo ya kodi ya ardhi. Makusanyo ya kodi ya ardhi yanayokusanywa na serikali za mitaa hugawanywa na Serikali kuu.

Katika mgao huo Serikali kuu hupata (70%) inayopelekwa hazina kuu na matumizi yake kuamuliwa na Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), wakati Serikali za Mitaa hupata 30%. Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa baada ya kushauriana na wadau wengine anaweza kuamua mgawanyo wa vyanzo vya mapato kwenye ngazi tofauti za halmashauri. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982.

Serikali za Mitaa hazina uhuru wa kujiamulia matumizi ya makusanyo yanayopatikina katika maeneo yao, badala yake ni lazima wapate idhini ya waziri ambae anatoka Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Kwa upande mwingine nchi zingine kama Kenya Katiba yao (ibara ya 209 na 210) imeweka mgawanyo wa madaraka ya kukusanya mapato na kodi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Ibara ya 202 na 203 ya Katiba ya Kenya inatoa mwongozo wa namna ya kugawa mapato kati ya Serikali mbili yaani Serikali kuu na Serikali za Mitaa. Ibara ya 187 na 176 zinatoa mwanya na nafasi kwa serikali kuu kupeleka baadhi ya majukumu yake (Serikali kuu) kwenda Serikali za Mitaa. Ibara ya 204 inatoa fursa ya mgawanyo sawa wa mapato na rasilimali kwa maeneo yaliyoachwa nyuma kiuchumi (marginalized).

Serikali za Mitaa zina nafasi kubwa sana katika usimamizi wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira. Ingawa Sheria za nchi zimetoa fursa na majukumu ya Serikali za Mitaa katika usimamizi wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira,lakini Katiba ya sasa haijasema chochote katika masuala haya muhimu kwa maisha ya binadamu. Katiba za nchi nyingine kama Kenya zimeweka bayana nafasi za Serikali kuu na Serikali za Mitaa katika usimamizi wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira.Hii inaonyeshwa katika ibara ya 69 na 70.

**Tunapendekeza** yafuatayo;

- Wakati tukiandaa Katiba mpya tunapaswa tuangalie namna ya kujifunza kutoka Katiba ya Kenya hasa mambo yaliyomo katika ibara ya 6 na ya 174. Umuhimu wa kuwa na Katiba yenye serikali ya ngazi mbili yaani Serikali Kuu (central Government) na Serikali za Mitaa (local government) zenye uhuru wa madaraka na maamuzi.

- Serikali za Mitaa zisiingiliwe na Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na ziwe na uhuru kamili wa kujiamulia mapato na matumizi yake ikiwemo wajibu wa kuchangia hazina ya Serikali Kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na makusanyo kwenye Serikali za Mitaa yatumike katika eneo husika.
- Ziwepo mamlaka/taasisi katika Serikali za Mitaa ambazo zitakuwa na jukumu la kukusanya mapato katika halmashauri.
- Serikali za Mitaa ziwe na vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya halmashauri husika na kuwa na uwezo wa kuandika bajeti ya halmashauri yake yenyewe na si kutegemea mwongozo wa bajeti kutoka serikali kuu (ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na sehemu ya mapato yake kupelekwa hazina kama ilivyo kwa sasa.
- Wakati tukiandaa katiba mpya tunapaswa tuangalie namna ya kujifunza kutoka Katiba za nchi zingine mfano katiba ya Kenya hasa mambo yaliyomo katika ibara ya 202 (kugawana mapato kwa haki na usawa-equitable sharing of revenue), 203 (masuala muhimu ya kuzingatia katika mgawanyo wa mapato ya Taifa mfano maslahi ya Taifa), 209 (mamlaka ya kutoza Kodi ya Mapato itafanywa na Serikali kuu tu) na ibara ya 210 (mamlaka ya kutoza kodi au ushuru yatokane na Sheria kuu-Parent Act).
- Umuhimu wa kuwa na katiba yenye Serikali mbili huru yaani Serikali kuu (central Government) na Serikali za Mitaa (local government) zenye uhuru wa madaraka na maamuzi.
- Katiba mpya iangalie mfano wa nchi zingine kama Kenya kwa kuweka bayana nafasi za serikali kuu na serikali za mitaa katika usimamizi wa ardhi na uhifadhi wa mazingira

- Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 18 (a-d), kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi, kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na pia kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

- Hata hivyo haki hii imekuwa ikikiukwa katika serikali za mitaa kutokana na kutokuwepo kwa Sheria ya Uhuru wa Habari. Ni katika sheria ya uhuru wa habari haki hii inaweza kupatikana ili aina ya habari zinazotakiwa kupatikana kwa umma ziainishwe na pia hatua zitakazochukuliwa kwa kiongozi ambaye atashindwa kutekeleza sheria hii.

- Viongozi katika serikali za mitaa wawekewe utaratibu wa kikatiba wa kuwawajibisha kutoa taarifa kwa wananchi pale wanapotakiwa ili kuimarisha suala la uwazi na uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi
- Kutekeleza ibara ya 8 (1) (a) ya katiba ya sasa ambayo inamtambua mwananchi kama msingi wa mamlaka yote, na kwamba serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.
- Utekelezaji wa ibara hii unarahisisha utekelezaji wa ibara ya 18 ya katiba ya sasa.
- sera ya Ugatuaji wa Madaraka (Decentralization by Devolution)itekelezwe ipasavyo ili sauti za wananchi na viongozi wa ngazi za msingi zisikike katika kupanga na kutekeleza mipango yote ya maendeleo ya Taifa letu kupitia O&OD na mbinu zinginezo.
- Michakato ya Mipango na Bajeti ianzie kwa wananchi na utekelezaji wao kutathminiwa na wananchi

- Halmashauri ziongezewe uwezo wa kukusanya mapato ili ziweze kujitosheleza kibajeti
- Wakaguzi wa ndani wa hesabu katika halmashauri, wakara za serikali, wizara na idara waajiriwe na Mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali (CAG) ili waweze kutekeleza shughuli zake ipasavyo
- Wenyeviti wa Serikali za Mitaa/vijiji wapangiwe posho kwa ajili ya majukumu yao
- Ukusanyaji wa kodi na mapato ya serikali uanzie kwenye ngazi ya nyumba kumi kumi ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha kuna ushiriki wa kila mwananchi
- Sheria ziweke utaratibu (to set standard) za kuonesha matumizi stahiki yanayoendana na thamani ya pesa (value for money); ufanisi (efficiency) na utumiaji bora wa pesa rasilimali za umma (effective use of public resources).

## SURA YA TISA

## MAJESHI YA ULINZI

Tanzania ina majeshi ya Ulinzi (JWTZ), Polisi, Magereza, na Uhamiaji. Pia kuna majeshi yasiyo rasmi kama vile Mgambo, Sungusungu, Green Guard (CCM), na Red Brigade (Chadema).

**Tunapendekeza** kwamba:

- Majeshi rasmi yaendelee kutambuliwa na kudumishwa kwa ajili ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu. Majeshi yasiyo rasmi (Mgambo, Sungusungu, Green Guard, na Red Brigade) yafutwe ili kuthibiti uhalifu na uwezekano wa machafuko ya kisiasa nchini
- Majeshi yote yasijihusishe na siasa wala chama tawala kisitumia mojawapo ya jeshi au majeshi kujilinda. Endapo ikionekana dalili hizo, mkuu wa jeshi hilo lazima ajiuzulu ndani ya saa 24.
- Jeshi au majeshi rasmi yasitumiwe na viongozi walioko madarakani kulinda nyadhifa zao au kukandamiza raia wasiounga mkono viongozi hao. Majeshi yatekeleze wajibu wao kwa mujibu wa sheria
- Kambi za majeshi zihame katika maeneo ya mijini karibu na makazi ya raia

# SURA YA KUMI

# MAONI MENGINE:

## *I. MAONI KUHUSU MAZINGIRA, MALIASILI NA UMILIKI WA ARDHI*

Kuna hitaji la muhimu kuingiza vifungu maalum vinavyohusu haki za mazingira, uhifadhi na menejimenti ya mazingira katika itakayokuwa katiba mpya. Hii italinda dhidi ya uwezekano wa kupitisha sheria za kisekta au urekebishaji wa sheria zilizopo kwa namna ambayo inadhoofisha haki ya kufikia, kuhifadhi, na kutunza mazingira iliyotolewa kwa wananchi. Hii inaendana na kanuni ya kuwa Katiba ni sheria kuu ambayo kwayo sheria nyingine zote sharti zikubaliane nayo.

**Tunapendekeza** kwamba:

- Kuna hitaji la kuingiza katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania vifungu vilivyoainishwa kwa umakini, kwa uwazi na vinavyotoa mamlaka ya ulinzi, uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira Tanzania kwa serikali na wananchi
- Inapendekezwa kwamba masuala ya haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na yenye afya, misingi ya menejimenti endelevu ya mazingira, majukumu na wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kutunza na kusimamia mazingira sharti yaingizwe katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

- Katiba itamke wazi kuwa rasilimali na maliasili za nchi ni kwa ajili ya watanzania na hivyo zitanufaisha watanzania zaidi ya wageni

- Katiba itamke wazi kuwa mikataba yote inayohusiana na matumizi ya maliasili ya nchi itakuwa wazi kwa kila mtanzania na itajadiliwa na bunge kabla ya kusainiwa

- Wageni wapangishwe ardhi kwa muda usiozidi miaka 50 au waingie ubia wa muda na raia katika matumizi ya ardhi ambayo raia halali wanamiliki. Lazima ardhi ibaki kwa mzawa. Serikali isaidie mikataba kati ya raia wa Tanzania na wageni.
  - Umiliki wa ardhi uhusishe na rasilimali zilizoko chini ya ardhi hiyo. Serikali ipewe sehemu ya mapato kwa mujibu wa sheria
  - Serikali ipime maeneo ambayo hayajapimwa na kuwamilikisha wakazi wa eneo wanapoishi ili kulinda haki zao na kuepusha migogoro ya ardhi nchini.
  - Katiba itamke wazi kuwa raia wa Tanzania ana haki ya kumiliki ardhi na hivyo kila raia ardhi yake ipimwe na kukabidhiwa hati ili kuondoa migogolo tunayoiona. Wananchi wasihamishwe kwa nguvu kutoka katika maeneo yao kwa sababu ya wawekezaji mpaka mijadala ya wazi inayohusisha wadau iwe imefanyika.
  - Ardhi ni mali ya watanzania wote na itatumika kwa njia endelevu kwa ajili ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo
  - Ardhi itatumika kwanza kwa ajili ya uhakika wa chakula wa nchi kabla ya kufikiria matumizi mengine
  - Matumizi ya ardhi kwa kazi yoyote ile ikiwepo kilimo na uvunaji wa maliasili yatahakikisha kuwa biaonuai ya nchi inatunzwa, kuhifadhiwa na kuendelezwa
  - Ardhi haitauzwa kwa mgeni yeyote Yule kama mtu binafsi, kampuni au taasisi

- Katiba iweke ukomo wa upangaji/ukosishaji wa ardhi kwa matumizi mbalimbali. Ardhi itakodiwa kwa kipindi kisichozidi miaka 50
- Watanzania hawatanyang'anywa ardhi kwa ajili ya wawekezaji bali watawezeshwa kuitumia ardhi hiyo
- Katiba itamke wajibu wa serikali kulinda rasilimali za Taifa kwa manufaa ya vizazi vijavyo.Uvunaji wowote wa rasilimali usiozingatia maslahi ya taifa usiruhusiwe.

- Haki ya chakula: Katiba itamke kuwa kila mtanzania ana haki ya kujipatia chakula cha kutosha (the right to be free from hunger and to adequate food of acceptable quality).

## II. HUDUMA ZA JAMII:

**Tunapendekeza** kwamba:

- Katiba Mpya itoe haki JUMUISHI, yenye UHURU na HAKI. Izuie UBAGUZI katika utoaji wa huduma za afya, mali na vifaa, Aidha afya lazima IPATIKANE, IPATIKANE KARIBU, IKUBALIKE KWA WATUMIAJI NA WATOA HUDUMA na iwe ya viwango vya JUU.
- Serikali inawajibu kuhakikisha huduma za afya ni za kiwango cha juu na kuwa serikali itahakikisha dawa za magonjwa sugu/msendeko zinapatikana wakati wote na ni haki ya kila mtanzania anayestahili kuzipata anazipata bila masharti
- Endapo serikali haitatimiza wajibu WA kulinda haki ya kuishi YA kila mtanzania, itaweza kushtakiwa kwa kosa hilo.
- Serikali itahakikisha kuwa kila mtanzania uhai wake unalindwa kwa namna yoyote. Hii ni pamoja naa kuwapeleka wagonjwa maskini nkatika hospitali zenye ujuzi stahiki kushughulikia magonjwa hayo.
- Katiba mpya isiwe na vifungu batili vinavyoinyima haki ya afya kwa mtanzania kama kile katika katiba ya sasa 7 (2).

## III.MUUNDO WA UTAWALA WA NCHI (MIKOA, WILAYA, TARAFA, KATA, VIJIJI, VITONGOJI, NYUMBA KUMI)

Utawala wa sasa una ngazi za Taifa, Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Vijiji, Vitongoji, Nyumba Kumi ambapo kuna viongozi wa aina mbalimbali sambamba kama vile:

*Rais →Mkuu wa Mkoa →Mkuu wa Wilaya →Katibu Tarafa→Katibu Kata→Mwenyekiti wa Kijiji→Mwenyekiti wa Kitongoji→Mjumbe wa Nyumba Kumi*

*→Katibu Tawala wa Mkoa→Katibu Tawala wa Wilaya→*

*TAMISEMI→Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya (DED) →*

**Tunapendekeza** kwamba:

- kwa kuwa mifumo sambamba inaongeza gharama za utendaji, nafasi za Wakuu wa Wilaya ziondolewe ili wabaki Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa watakaosimamiwa na wananchi wenyewe na madiwani na TAMISEMI. Uenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wa wilaya ibaki kwa mkuu wa polisi wa wilaya.
- wakurugenzi wa halmashauri wapate nafasi hizo kwa kuomba TAMISEMI
- Mfuko wa maendeleo ya jimbo ufutwe maana ni kinyume cha sheria na unamnyanganya mbunge nguvu ya kuhoji endapo hatakuwa ametumia vizuri fedha za mfuko wa jimbo.

## IV. TUME MBALIMBALI

Tunapendekeza katika uteuzi wa tume mbalimbali Rais awajibike kuhakikisha taarifa za tume zote zilizoundwa zinatolewa kwa umma siku thelathini baada ya tume kukamilisha uchunguzi wake. Hii ni kwa sababu Tume zote hutumia rasilimali za wananchi lakini hazina manufaa kwa wananchi.